

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUANZA KUTUMIKA KWA SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA MANISPAA YA KINONDONI ZA MWAKA 2018.

Tarehe 29/10/2019.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni itanza rasmi kutumia Sheria ndogo za (Ada na Ushuru) za Manispaa ya Kinondoni za Mwaka 2018 kuanzia Ijumaa tarehe 01/11/2019 baada ya kupitishwa na Baraza la Madiwani na Kukubaliwa rasmi na waziri mwenye dhamana (Waziri wa TAMISEMI) kwa ajili ya Utekelezaji baada ya Kukamilisha hatua zote muhimu za Mijadala mbalimbali ya muda mrefu kwa Kushirikisha wadau wote muhimu wa Manispaa kuanzia tarehe 02/10/2018 katika Ukumbi wa Manispaa ya Kinondoni ikihusu Ada ya Ukaguzi wa nyama, Ada za leseni za eneo, uchunaji wa ngozi na upangaji wa madaraja na Ada ya kusajili kituo cha kuoshea wanyama (Josho) na kutunza wanyama waliojeruhiwa na kutelekezwa.

Kwa mujibu wa Sheria hizi Ndogo, Ada ya ukaguzi wa nyama kwa machinjio binafsi kwa kila ng'ombe mmoja ni Tshs.3,000/=, Kwa kila mbuzi/kondoo ni Tshs.1500/= kwa kila nguruwe ni Tshs.1500/= kwa kila kuku mmoja na jamii ya ndege ni Tshs.50/=, Wakati Ada kwa machinjio iliyojengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuchinjia wanyama, kuku na jamii ya ndege itatozwa kwa mujibu wa Mkataba.

Aidha Ada ya lesseni ya uchunaji wa ngozi na upangaji wa madaraja kwa mwaka ni Tshs.20,000/=, Ada ya lesseni ya eneo kwa mwaka ni Tshs.50,000/= na Ada ya usajili wa Kituo kwa Mwaka ni Tshs,200,000/= kwa kila kituo.

IMETOLEWA NA:-

Sebastian M. Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.**